

# **Kudhibiti sumu kuvu kwenye mahindi kabla na wakati wa kuvuna**

Mawazo tofauti ya kulinda mahindi dhidi ya sumukuvu huwasaidia wakulima kabla na wakati wa kuvuna.

Sumu kuvu ni hatari kwa watu na wanyama. Ikiwa unalisha wanyama wako na chakula ambacho kimeathiriwa na Sumu kuvu, uzalishaji wa maziwa, mayai na nyama utakuwa chini. Pia binadamu anaweza kuathiriwa na sumu kupitia kula bidhaa hizo, na hivyo sumukuvu itashambulia maini na figo.

## **Ukungu ambaao huzalisha Sumukuvu**

Ukungu ambaao huishi ardhini na kula mmea unaweza kuzalisha Sumu kuvu. Upepo hueneza ukungu ambaao kutua kwenye nyuzi za gunzi la mahindi. Baadaye, ukungu hukua ukishambulia punje ambapo Sumu kuvu hukua.

Mahindi yana uwezekano mkubwa wa kushambuliwa wakati halijoto ni moto. Mahindi machanga huathirika zaidi na ukame.

## **Kulinda mahindi dhidi ya ukungu**

Ni muhimu kuanza kupanda hivi karibuni, ili kuepuka mimea yako kufa kwa sababu ya ukame. Unapopanda mahindi yako, panda mikunde kama mbaazi karibu na nayo.

Mbolea ni muhimu kwani hudumisha unyevu wa udongo. Kukatakata mabaki ya mimea shambani kunaweza pia kuwa muhimu. Tumia mitaro ili kudumisha unyevu.

Mara tu mahindi yanapokomaa, anza kuvuna. Unapaswa kuvuna wakati wa jua, kwa sababu vinginevyo ukungu unaweza kutokea kwenye mahindi yeye unyevu yaliyovunwa. Baada ya kuondoa maganda, mahindi yanapaswa kuhifadhiwa moja kwa moja kwenye mfuko, ili kuepuka mgusano na udongo. Ondoa na kuchoma kila mahindi yaliyoshambuliwa.